# KULIONGOZA
# KANISA KWA WAKATI UJAO WENYE NGUVU

*Maarifa ya Uongozi na Washa za Mafundisho*

**Kitabu cha Kwanza kati ya vitano**

Huduma ya Dynamic Churches International

Dynamic Churches
International

Mungu ametupa fursa ya ajabu ya kukutumikia wewe, kanisa lake. Tamaa yetu ni kukusaidia uweze kupata wanafunzi wengi walio bora. ***Dynamic Churches International*** **(Makanisa ya kimataifa yenye nguvu)** ni shirika lisilo la kibiashara.

***Maono yetu ni kuwafanya wakufunzi wa kutosha kuwasaidia wachungaji na viongozi wa Kikristo kuwa na makanisa yakutosha yenye kufanya wenye nguvu. watakaoweza kuifikia jamii katika nchi zote za ulimwengu na injili ya Yesu Kristo.***

Ninaomba ya kuwa vipindi hivi vya uongozi na Washa za mafundisho zitakusaidia kusitawisha maono yako, ufahamu, ustadi na ujasiri ili uanzishe **huduma ya kufanya wanafunzi wa kimataifa** itakayogusa maisha ya wengi katika jamii yako na upendo wa Kristo. Ninahakika ya kuwa Mungu ametuleta pamoja katika wakati huu wa maana katika historia. Kama Wakristo tunalo jukumu la kufanya katika mpango mkuu wa Mungu katika dunia hii. Maneno ya mwisho ya Yesu kwa wanafunzi wake na kwetu sote yalikuwa ni kwenda na kuwafanya wanafunzi mataifa yote.

(Mathayo 28:18-20) Amri kuu itatimia tunapoyafuata maagizo yake ya Biblia.

Tamaa yetu ni kukusaidia wewe binafsi na kanisa kuyatimiza yale Mungu aliyokuitia kutimiza ili Mungu atukuzwe zaidi.

Al Middleton

**Al Middleton**
**Mkurugenzi wa Kimataifa**

## Jinsi ya kutumia Kitabu Hiki Cha Mafundisho

Mafundisho haya yameundwa yawe na urahisi wa kufundisha ili wale utakao wafundisha watakapo kuwa na muundo wa kufanya wanafunzi, wataweza kufundisha wengine (Kuzaa)

Kuna njia nyingi za kutumia kitabu hiki. Yafuatayo ni maoni:

1. Kisome mara kadhaa ili uelewe kisha uanzishe kundi lako dogo na ufanye wengine kuwa wanafunzi kama ilivyoelezwa katika kitabu hiki.

2. Ikiwa wewe ni mchungaji, shiriki pamoja na viongozi wako wa kanisa. Wakitaka anzisha makundi madogo pamoja nao na uwafundishe Mmoja kwa Mmoja. Watazaa wawe watu wengi zaidi.

    - Unapokuwa na viongozi wapya ambao wako tayari kuanzisha vikundi vyao, inabidi uwafundishe mafundisho haya mmoja kwa mmoja au kwa vikundi ili waweze kuelewa au kufahamu mafundisho ya jinsi ya kuwa kanisa linalofanya wanafunzi.

3. Mnapozidi kuwa na makundi mengi na kuwa na wanafunzi wengi, wachungaji wengine watataka uwasaidie kufanya hivyo katika makanisa yao. Panga wakati wa viongozi wao. Baadhi ya watu wako wanaweza kusaidia kufundisha watu wao.

4. Husisha makanisa mengine juu ya maono haya mpaka kuwe na washuhuda wengi watakaoweza kuifikia jamii yako na injili ya Yesu Kristo.

**Namna ya Kufundisha:** Katika kila kipindi eleza maana ya picha zilizochorwa kisha mjadiliane na ujibu maswali unaposoma maandishi hali ukisisitizia sehemu muhimu.

**Usiongezee** mawazo mengi kwani yanaweza kutatiza na kuchanganyisha. Pia itapunguza uzao wa mafundisho haya. **Shiriki shauku yako na msisimko wako mwenyewe** katika mambo ufundishayo. **Hakikisha kutoa mifano ya watu binafsi jinsi Mungu alivyogeuza maisha** (yako na watuwengine) katika kutumia kanuni hizi.

Vipindi vitatu vya ***Maarifa ya Uongozi*** vimeundwa ili vijenge filosofia na maarifa ya kuwa kanisa la kufanya wanafunzi. Kila kipindi cha maarifa kitachukua muda wa **saa moja na nusu ya mazungumzo.**

Washa z*a* ***jinsi ya kuanzisha*** hutoa maagizo kwa mchungaji/kiongozi jinsi ya kuwapa viongozi wake ujuzi wa kufaa kazi na kumjulisha kwenye Makundi Madogo na Mafundisho ya Mmoja- kwa-Mmoja ***Misingi Yenye Nguvu, Ukufunzi Wenye Nguvu na Ushirika Wenye Nguvu.***

# Kuliongoza Kanisa kwa Wakati ujao Wenye Nguvu

Kitabu hiki ni kimoja katika mfululizo wa mafundisho katika ***Kuliongoza Kanisa kwa Wakati ujao Wenye Nguvu.*** Ukurasa ufuatao unaonyesha jinsi **Maarifa ya Uongozi na Washa za Mafundisho** zinavyoingiliana **Katika Maarifa yote ya Kujenga Watu:**

| Kitabu cha mafundisho | Mafundisho ya |
|---|---|
| 1. **Maarifa ya Uongozi** <br><br> **na** | - **Wachungji na viongozi katika elimu ya kujenga kanisa lenye ufanya wanafunzi** |
| **Washa za Mafundisho** | - **Wachungaji na viongozi kwenye Jinsi ya kufanya wanafunzi katika Makundi Madogo na ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja.** |
| 2. Kujifunza kuongoza mafundisho ya kiongozi mwanafunzi | - Viongozi wa makundi ya uhai watumie katika kuwafundisha viongozi walio wanafunzi. |
| 3. Viongozi wanaongoza mafundisho ya viongozi wa makundi ya uhai | - Waalimu wayatumie kwa mafundisho ya viongozi wa makundi ya uhai. |
| 4. Kundi linaloshinda kujenga waalimu na vifaa. | - Wachungaji wayatumie katika kujenga waalimu wao. |
| 5. Kuongoza hadi mbele mafunzo ya mchungaji kwa mchungaji | - Wachungaji na viongozi wanaotaka kuwasaidia wengine wajenge njia ya kufanya wanafunzi katika kanisa lao la nchini au kimataifa. |

Vifaa hivi vyote vyapatitaka kupitia kwa afisi yetu kwa anwani ifuatayo.

***Dynamic Churches International***

Simeon Oyugi – Kenya Rep.
P O Box 798-00515
Buruburu, Nairobi,
Kenya East Africa
Email: ncc_africa@yahoo.com

Al Middleton - Executive Director
164 Stonegate Close
Airdrie, Alberta T4B 2V2
Canada
dcioffice@shaw.ca

Vifungu vyote vya maandiko vilivyonakikiliwa katika chapa hii ni kutoka kwa Biblia Habari Njema toleo la 1995, na ile ya muungano wa kimataifa wa mashirika ya Biblia 1994, 1952, 1989

Hakuna ruhusa ya kutoa nakala hizi kwa matumizi ya kibiashara lakini unaruhusiwa kutoa kwa matumizi ya kibinafsi pekee.

© 2016 Dynamic Churches International
Haki zote zimehifadhiwa

# Maarifa ya Uongozi
# na Washa za Mafundisho

## *Yaliyomo*

## Vipindi vya Washa za Uongozi


| **Kichwa** | **Ukurasa** |
|---|---|
| Mpango wa Mungu kwa Kanisa Lake ni Nini? | 1 |
| Muundo wa  Kanisa Lifanyalo Wanafunzi | 13 |
| Kustawisha Hali ya Mfululizo wa Kufanya Wanafunzi | 23 |


## Namna ya Kuanzisha Washa


| | |
|---|---|
| Washa ya Mazoezi ya Kundi la Kwanza | 38 |
| Washa ya Maagizo ya Misingi Yenye Nguvu | 47 |
| Washa ya Maagizo ya Ukufunzi Wenye Nguvu | 48 |
| Washa na Maagizo ya Ushirika Wenye Nguvu | 49 |
| Bidii ya Kiongozi | 51 |
| Cheti cha Kuhitimu | 52 |


***"Kuongoza Kanisa Kwenye Maisha Yajayo ya Nguvu"***

# *Mpango wa Mungu kwa Kanisa Lake ni Nini?*

***"Kuongoza Kanisa Kwenye Maisha Yajayo ya Nguvu"***

# Mpango wa Mungu kwa kanisa lake ni nini?

Kipindi hiki chatoa lengo la Biblia kwa kanisa.  Ndio msingi wa mafundisho yote.

**Mwito Mkuu**

***"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.  Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*** **Mathayo 28:18-20**


**Mwito Mkuu wasema, "fanya wanafunzi wa mataifa yote".**

***Mwanafunzi ni nini?***
Ni mtu aliyempokea Kristo na kufuata mafundisho yake

***Wanafunzi hufanyikaje?***
Sharti tuwe wanafunzi kisha tuwafanye wengine kuwa wanafunzi kwa:

- **Kuenenda (uinjilisti)**
- **Kubatiza (Kujitambulisha na Kristo katika kifo chake, kuzikwa na kufufuka kwake) na**
- **Mafundisho ya kutii ukufunzi.**

## Kufanya Wanafunzi ni Mfululizo wa Kuendelea




## Kufanya Wanafunzi Ndicho Kiini cha Kanisa kwa Maana Ndicho Kiini cha Mwito Mkuu

## Enenda

***Maana ya kuenenda ni nini?***
Siku sita za juma sisi (kanisa) tuko nje duniani (Kazini, shuleni, mtaani)

- Yatupasa tuwe chumvi na nuru ya ulimwengu.

- Kanisa la kwanza walieneza injili kila mahali walipoenda na siku hizi Wakristo wengi hawajashiriki imani yao na mtu yeyote.

**Kwa nini Wakristo wengi hawaenendi?**

1. Huenda hawana ufahamu/ujuzi wa ukweli wa maisha ya Kikristo ya kila siku.

2. Hawana mengi ya kushiriki kwasababu hawajafunzwa kutii amri za Kristo.

- Wakristo wengi hawajui jinsi ipasavyo kushiriki imani yao - wanahitaji kufundishwa.

## Batiza

Wote wampokeao Kristo kama mwokozi wanahitaji kuelewa maana ya kujitambulisha na kifo cha Kristo, kuzikwa, na ufufuo wa maisha mapya.

Ili tuweze kuishi maisha ya Ukristo wenye ushindi tukiwa wana wa Mungu, yatupasa kufahamu ujumbe wa injili wa sisi ni nani **katika Kristo.**

***Basi, Yesu akawaambia wale wayahudi waliomwamini,"kama mkiyazingatia mafundisho yangu mtakuwa kweli wanafunzi wangu. Mtaujua ukweli nao ukweli utawapeni uhuru.***
**Yohana 8:31,32**

Sote tunatamani kuwa huru. Shetani anataka sisi tufikirie ya kuwa tumo kifungoni wala hatuko huru. Kuukubali ukweli wa neema ya Mungu na kuishi kwa ukweli wa Mungu, sio uwongo wa shetani utakuwezesha kuishi katika uhuru ulionao ndani **"ya Kristo"**. Kama umempokea Kristo kama Mwokozi wako uko huru kweli kweli!

Kama Mkristo yanipasa kujua, kufahamu na kukubali ukweli wa Mungu unaonihusu.

3. Nime **kubalika** katika Kristo
4. Niko **salama** katika Kristo
5. Nina **maana** katika Kristo

# ***Kama umempokea Kristo kama mwokozi wako, uko huru kweli kweli!***

# Fundisha Utiifu

**Maana ya kufundisha ni:**

- Lazima kuwe na utangulizi mzuri (Upendo, ushirika, kukubalika, kudiriki na **ibada** kwa Mungu.) Ni lazima uufurahie wakati wako pamoja na waamini wengine.

- Kila mtu ni lazima aondoke akiwa amehudumiwa na anafurahia kufanya ukweli mpya katika shughuli zake za kila siku.

- Makanisa hayawezi kufundisha neno tu (Ukweli wa Mungu wa ndani) bali ni lazima **"wafundishe utiifu".**

**Kutii ni:**


- Kufanya ukweli wa Mungu maishani mwetu. **Ukufunzi ni kuishi kama Kristo, wala sio kujifunza mambo ya Kristo.**

- Kwenda na kumshuhudia Kristo. Siku ile kanisa la kwanza lilipoanza, watu 3000 walimpokea Kristo kama mwokozi wao, kisha wakaendelea kuwafundisha hawa waamini wapya jinsi ya **kutii** amri zote za Kristo.

Kwa ufupi mwito mkuu wasema, "**fanyeni wanafunzi wa mataifa yote watakaoenda na kumshuhudia Kristo kwa kila mtu katika mataifa yao ambao pia watamshuhudia Kristo katika mataifa mengine".**

## Usawa ndiyo Funguo

Uwe na usawa kati ya **"Kuenenda"** na **"Kufundisha kutii".**




## Kujitambulisha Kwako kwa Kristo ndio Msingi Wako

# Anza Ukiwazia Mwisho:
# Mwito Mkuu

Je, unaamini mwito mkuu? ________________________ndiyo ___________________la

Je, umewahi kuzingatia maana ya kutimiza mwito mkuu?

Kama mwito mkuu ungetimizwa, ungeonekanaje? Nakili baadhi ya mabadiliko katika mtaa wako ambayo unaamini yangepatitakana katika kutimiza mwito mkuu:

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

## Je, unayo maarifa thabiti ya kutimiza Mwito Mkuu?

Kama huna, je, bado unaamini ya kuwa mwito huu mkuu ni wako na waweza kutekelezwa?

## Maono

Mpango wa Mungu ni kuwa kila kanisa lifanye wanafunzi wengi mashahidi watakaoweza kufikia kila mtu katika jamii zao na injili ya Yesu Kristo.

## Je, unaamini maono haya kwa kanisa lako? ____ Ndiyo _____ La

## Mpango na maarifa

Mungu peke yake ndiye ajuaye jinsi mwito mkuu utakavyotimizwa bali wewe huenda ukataka kutumia mwongozo ufuatao utakaokusaidia kujenga maarifa yako ili utimize maono yako.

**A.** ______________ = Idadi ya watu katika Jamii/Mitaa yetu. Kama kila mwanafunzi angeshuhudia watu 9 (1 kwa 10) tungehitaji: A ÷ 10 = B

**B** ______________ = Wanafunzi mashahidi kuifikia Jamii/Mitaa yetu.

**C.** ______________ = Idadi ya makanisa ya uinjilisti katika Jamii/Mitaa yetu: B ÷ C = D

**D.** ______________ = Wastani ya wanafunzi washahidi wanaohitajika katika kila kanisa

## *Inawezekana kwa kanisa letu kuzaa D ___________ wanafunzi mashahidi?*

# Jinsi inavyoweza kufanyika

Sasa waweza kuanzisha kikundi kitakacho kukua mpaka kifike watu 10

Kama utafundisha kila mshirika aweze kuishi na uhuru katika Kristo na watu 8 kati ya 10 waelewe na kudai haki zao katika Kristo kisha wafundishwe jinsi ya kushiriki imani yao, **je,** yawezekana kwamba watu 4 kati ya 10 wangekuwa wanafunzi mashahidi na kumshuhudia Kristo na watu 9 wengine? _________ Leo hii kuna mkristo 1 kati ya 9 wasio wakristo ulimwenguni.

## *Ni makundi mangapi tungeliyahitaji katika kanisa letu?*

**D** _____ ÷ 4 wanafunzi mashahidi katika kila kundi = E___________ (idadi ya makundi yanayohitajika kufika kanisa la wastani). Kanisa lako laweza kuhitaji zaidi au machache.

## *Twawezaje kuongeza makundi ya E*?_________________

## Yawezekana! Yawezakuwa namna hii:

Kama tungeanza leo na kundi moja kisha kila kundi lingeongezeka kuwa makundi mawili.

**1** x 2 **= 2** x 2 **= 4** x 2 **= 8** x 2 **= 16** x 2 **= 32** x 2 **= 64** x 2 **= 128** x 2 **= 256** x 2 **=512** x 2 **= 1024**

Piga mviringo kwa makundi yote katika msitari wa juu ambayo tungekuwa nayo. Idadi ya vizazi ambavyo vingehitajika kufikia lengo letu la makundi **E** _________ ni __________

**Kwa mfano:** ***Kama tungehitaji makundi 60, ingechukua vizazi 6 vya kuongezeka (Kila kundi likiongezeka kuwa makundi 2) Kila kizazi kingechukua Takriban miezi 6.***

Mafundisho yaliyobaki yameundwa kuwapa viongozi wetu wa kanisa maarifa rahisi yenye nguvu yawezayo kufanya kanisa lenye kufanya wanafunzi.

Mwito mkuu unahusu idadi ya watu ulimwenguni kote. Yaweza kutimizwa na Roho wa Mungu kwa **uhusiano wetu na watu wengine!**

# Kanuni za Kukua

## Jamii ya Kawaida

Hebu tuone jinsi tunavyokuwa kimwili.

**Uzaliwa ⇒ Mtoto ⇒ Kijana ⇒ Mtu Mzima ⇒ Aliyeoa/olewa ⇒ Kitoto ⇒ Mtoto ⇒ Kijana**

Kukua hufanyika vizuri katika jamii, lakini yahitaji ulezi wa Mmoja-kwa-Mmoja na mafundisho.

---

## Jamii ya Kiroho

Ukuzi wa kiroho hufanyika vyema kwa njia ya **jamii ya kiroho.** (Kundi dogo) Lakini lahitaji utunzaji na **mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja**

**Mkristo Mchanga ⇒ Mwanafunzi ⇒ Mwalimu ⇒ Kiongozi ⇒ Mkristo Mchanga ⇒ Mwanafunzi ⇒ Mwalimu**

Mtu huonyesha ishara za **ukomavu** anapoacha kujipendelea **mwenyewe** na kuangalia mahitaji ya wengine.

## *Kanisa Lapaswa Kuwa Umoja wa Jamii za Kiroho!*


**Makanisa mengi yamefanana na nyumba ya kutunza na kulea mayatima wa kiroho kuliko kuwa jamii ya kiroho.**

**Mayatima wa kiroho __________________________________________ Jamii ya Kiroho**

Weka alama "**X**" katika Msitari uliofanana na kanisa letu. Weka alama "**O**" mahali unataka liweko.

# Mfululizo wa Kufanya Mwanafunzi

Ili tuweze kuwa **jamii ya kiroho** inayokuwa, itatupasa kuunda **Njia ya Kuwafanya Wanafunzi. Njia** iliyo na kanuni za Biblia za miviringo hii minne yapasa kuundwa ili kusaidia kukamilisha lengo letu na kutimiza mwito mkuu.




Soma picha hii na uifuatishe mishale unaposoma maelezo yafuatayo.

**Mfululizo huanza  na mpango wa Mungu tunapo....**

## Shiriki injili ya Yesu Kristo na watu wengine

Hili **ndilo lengo la Mungu kwa kanisa lake** na ni sharti liwe lengo letu daima!

***Kwanini?*** ______________________________________________________

***Sababu gani zinazofanya kanisa kuacha kufikia watu wapya na kumshuhudia Kristo?***

_____________________________________________________________

***Tutawafanyaje watu hawa wanaompokea Kristo kama Mwokozi wao?***

## 1. Wakristo wapya wanahitaji malezi baada ya kuwafikia.

**Sharti tuwalee kwa kuwapenda na kuwatunza**

***Mfululizo unaendelea tunapo*....**

## Wafundishe wakristo wapya misingi ya Ukristo.

Maombi na mafundisho ya Biblia ndiyo Misingi. ***Ni misingi gani mingine ambayo Mkristo mpya anapaswa kuielewa?*** ______________________________

______________________________

______________________________

Kuna umuhimu gani kwa watu wapya kufundishwa misingi ya Ukristo? ______________

______________________________

## *2.* Wanafunzi Wafundishwa

***Kwa sababu wanafundishwa katika njia ya uzazi wana.....***

### *Fundishwa Kuzaa*

Wazazi ni watu wanaokuwa waalimu baada ya hao kufundishwa. Sasa wamehitimu kuwa viongozi.

## 3. Waalimu Wafundisha Wengine

Wale wanaozaa kwa kuwafundisha wengine katika misingi ni waalimu.

### *Ujenzi wa kiongozi na kazi yake.*

Baada ya kujidhihirisha kuwa***"Waaminifu na kuweza kufundisha"*** (II Timotheo 2:2), wako tayari kwa mafundisho zaidi ili waweze kutumika kwenye huduma maalumu.

***Mfululizo hupanuka wakati waalimu hawa wazazi wanapokuwa.......***

## 4. Viongozi Wanaopanua Huduma.

**Tahadhari:** ***Katika kila sehemu ya mfululizo mkazo ni katika kushiriki injili ya Yesu Kristo na wengine!***

Na mkono wako, funika yote isipokua miviringo ya 1 na 4 kwenye mchoro. Miviringo ya 1 na 4 yaonyesha jinsi makanisa mengi yanavyofanya kazi. Yakifikia watu wapya, huwaingiza kwenye huduma. Bila miviringo ya 2 na 3 watu hawatajengwa kama viongozi. Vyeo vya huduma vitajazwa na watu ambao pengine hawana uhakika na wokovu wao wenyewe. Pengine hawajui namna ya kuzungumza na Mungu katika maombi na kusoma Biblia. Huenda wasijue jinsi ya kujazwa na Roho Mtakatifu na ni **bahati kama watashiriki injili ya Kristo na Wengine!**


***Je, wafikiria huduma zao zitafaulu kiasi gani?*** ______________________

***Je, hii yaeleza juu ya (ma)kanisa yetu/letu?*** ______________________

## Njia ya Kufanya Wanafunzi Yahitajika Kutimiza Mwito Mkuu.

# Nia ya Uzazi
# Mtiririko wa Watu

| **Kuvutia** | **Uhusiano** | **Uzao** | **Muongezeko** |
|---|---|---|---|
| na kupendeza kwa huduma ya nje huleta watu wapya | ndio hufanya watu wapya kudumu | wa watu waliofunzwa ndivyo jinsi kanisa linavyokuwa | wa viongozi huleta matokeo ya kanisa linalokuwa na lenye kufanya wanafunzi |



***Ungelipimaje* kanisa letu kwa kila moja ya haya yaliyo hapo juu katika kipimo cha 1 kwa 10? (**1 chini, 10 juu)

______________ Mvutio wa huduma ya nje

________________ Uzao

______________ Uhusiano

________________ Mwongezeko

Angalia ya kwamba misitari kwenye mchoro ulio hapo juu ni myembamba katika sehemu ya uzao kwa sababu kujitolea zaidi kunahitajika wakati huu hili uyamimine maisha yako kwa maisha ya mtu mwingine.

## Uzao Ndio Ufunguo wa Kufanya Viongozi!

# Kukuza Desturi ya "Uzazi"

## Mvutio wa huduma ya nje husababisha watu wapya kuja.

Sababu ya kwanza watu huja kwa Kristo na kanisani ni uhusiano wa **kibinafsi**.

***Ni mkristo wa aina gani angemwalika rafiki yake?*** ________________________

***Je, watu wetu huwashuhudia na kuwaalika marafiki kuja?*** __________________

***Kama ni la, kwa nini basi?*** __________________________________

## Uhusiano hufanya watu wapya kukaa.

Watu husema, ***"Nahitaji jamii na uhusiano mzuri"***

***"Huduma huendelea katika uhusiano!"*** ( Al Broom.)

Mtu wa wastani anayetembelea kanisa anahitaji mguso wa watu 7 katika juma la kwanza, ama sivyo huenda anaweza kwenda mahali pengine.

> ***Katika mda wa miezi 12 iliyopita, wadhania ni watu wangapi waliotembelea kanisa letu?*** _______ ***Wadhani ni wangapi waliokaa nasi?*** ____________

***"Watu hawajali ufahamu wako mpaka wajue jinsi unavyohusika nao".*** John Maxwell

## Uzao - wa watu waliofunzwa ndio jinsi kanisa linavyokua

***Uzao ni nini?***
Kuzaana ni mtu mmoja anapomfundisha mtu **mwingine** katika hali ya kuwa yeye naye aweze **kumfundisha** mwingine atakayefanya vivyo hivyo katika mambo yote ya huduma katika kanisa letu.

***"Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia."***
2 Timotheo 2:2

***Kuna umuhimu gani katika kuzaana?***

> **Kuzaana** ndio **CHANZO** cha kukuza **viongoz**i.
> **Kukuza viongozi** ndio **CHANZO** cha kanisa lenye **kufanya wanafunzi**
> Kazi ya washangiliaji kanisani ni kula tu. Kuzaana ni kujifunza **kutoa**.

***" Kama wewe huwafundishi wengine ili wafanye yale unayoyafanya, basi unayoyafanya ni kazi bure!"*** Dr. Howard Hendricks.

***Kuzaana (kuwafundisha wengine wazaane) huanzia wapi?*** ______________________

______________________________________________________________________

***Kwa nini uanze na watu wapya*** _____________________________________________

***Kiasi gani cha wakati wao kinachopaswa kutumiwa katika kiwango cha uzao na wachungaji wengi na viongozi?______% Kwa nini iwe ya umuhimu zaidi?***

_______________________________________________________________

***Matokeo ya kuwakuza na kuwastawisha viongozi ni kanisa linalofanya wanafunzi***

Leo hii viongozi wengi wa kanisa hutumia asilimia tano (5%) ya wakati wao na bidii zao kwa kujizalisha wenyewe.

**Kuongezeka kwa viongozi hutokana na kuzaana.**

# Muhtasari

***Je, Wakristo huwezaje kuimarika katika kujitambulisha kwao na Kristo?***

Kupitia kwa **kujua, kufahamu** na **kukubali ukweli** kuhusu sehemu yao na kujitambulisha ndani ya Kristo.

***Kanisa hukuaje?*** (angalia ukurasa 10)
Katika kiroho____________________ na takarimu.
Kuzaa ni jinsi ____________________wanavyokuzwa

**Ukuaji hutokea vizuri katika mpango wa jamii ya kiroho.**

***Kanisa laweza kukua liwe kubwa kulingana na uthabiti wa misingi yake.***

***Pasipo ukweli wa Mungu, uhusiano sio thabiti.***
***Pasipo uhusiano wenye lengo, viongozi hawawezi kukuzwa.***
***Pasipo viongozi, kanisa haliwezi kukua.***

# Kanisa Letu Lawezaje Kuundwa Ili Tuweze Kutekeleza Mfuatilio wa Kufanya Wanafunzi?

# Muundo wa Kanisa Lifanyalo Wanafunzi

***"Kuongoza Kanisa Kwenye Maisha Yajayo ya Nguvu"***

# Kuwa Kanisa Lenye Kufanya Wanafunzi

Ulimwengu wetu wabadilika kila siku nalo kanisa lapoteza mguso wa ulimwengu huu unaobadilika. Makanisa mengi leo yako vile yalivyokuwa miaka 20, 50 na hata miaka 100 iliyopita. Wasiookoka wanaposema ya kuwa Ukristo si wa maisha yao, twakosa kutilia maanani jambo hili nasi twasema ya kuwa hawaitikii injili. Haisemi kwamba ujumbe wa injili wapaswa kubadilika bali yatupasa kuangalia matokeo yake.

***Mbona hatufikii ulimwengu wetu?***

Twahitaji kubadilisha jinsi tunawasilisha injili kwa ulimwengu wetu unao badilika.

***Mbona Tusiendelee Jinsi Tulivyo?***

1. Watu wanaoishi nje ya Kristo hawamletei Mungu heshima.

2. Wanapookoka na kukua ili wakomae ndipo watakapoweza kumheshimu na kumtukuza Mungu.


3. Ili kanisa litimize kusudi lake, ni lazima lijulikane kama watu wanaokuwa na kuwasaidia wengine wapate mabadiliko kupitia kwa nguvu za Kristo aliyefufuka.

***" Kuwa mwanafunzi na kufanya wanafunzi ni jibu la upendo kwa neema ya Mungu!"***

# Kanisa Letu Lahitaji Muundo Utakaotuwezesha Kuwafanya Wengine Kuwa Wanafunzi.

## *Kwa nini makanisa mengine hayana bidii?*

Mara nyingi mchungaji au mwanzilishi wa kanisa na viongozi hawafanyi wanafunzi, kwahivyo huduma yao iko vile ambavyo wao wenyewe wanaweza kufanya.
Mchungaji aliye onyeshwa hapo chini anafanya Huduma, lakini yeye hatayarishi wengine kwa Huduma.
Kwa sababu hiyo mahitaji ya watu kanisani hayashughulikiwi, na watu katika jamii hawatafikiwa kamwe!




**Mchungaji na wasaidizi wake wanatarajiwa KUFANYA kazi ya huduma.**


# Pasipo "*Kuwafanya Wanafunzi*" Je Kanisa Litaweza Kuufikia "Ulimwengu" Wake Kwa ajili Ya Kristo?

## *Yampasa Mchungaji na viongozi kufanya nini?*

Mfano wa maandiko:

***" Ndiye aliyewapa watu vipawa: wengine manabii, wengine wawe waeneza injili, wengine wachungaji na waalimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo,"*** Waefeso 4:11,12

**Mchungaji huyu anafundisha anapofanya huduma.**




Katika mchoro huu mchungaji anawafundisha viongozi ili waweze kuwafundisha wengine. Anapofanya hivyo, viongozi hawa wanaweza kutekeleza mahitaji ya watu wote kanisani. Pia wanaweza kufikia wengi katika jamii na mataifa mengine ya ulimwengu.

Paulo akamwandikia Timotheo:

> ***"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."***
> **2 Timotheo 2:2**

# Mchungaji na Viongozi Sharti Wafanye Wanafunzi!

# Je, Wawezaje Kufanya Wanafunzi?

## Jukumu La Mchungaji na Viongozi

**Kutoa Uongozi Wa Kiroho**
- kutoa uongozi wa utauwa
- kufundisha ukweli wa mungu
- kuwasaidia watu wa mungu wajifunze kutii na kutekeleza ukweli wa biblia.

**Kuwafundisha Washirika Kwa Ajili Ya Kazi Ya Huduma**
- kama viongozi, yawapasa muwe na huduma kamilifu.
- utawaongoza wengine kwenye umbali unaoweza kuufikia wewe mwenyewe.
- mafundisho yatawatayarisha ninyi kama viongozi muweze **kuwaongoza** wengine.

**Soma Waefeso 4:11, 12**
- mfano: yesu aliwalisha watu elfu 5,000 vipi? Alimega mkate na samaki na kuwapa wanafunzi wake nao wakawapa watu.
- kulikuwa na **viongozi** wa kutosha, hatimaye kila mmoja akaondoka akiwa **ameshiba**.

## Jukumu La Washirika

**Fanya Kazi Ya Huduma**

**Wafundishe Wengine**
- unapojifunza uongozi thabiti waweza kuwafundisha wengine (kaa pamoja nao) ili uwasaidie kutimiza lengo la kanisa.

**Soma 2 Timotheo 2:2** kuna vizazi 4 vya **uzao** hapa!


**Paulo** ➔ **Timotheo** ➔ **Watu waaminifu** ➔ **Wengine pia**

Andika majina hapo chini likiwemo jina lako kama waweza kutambua vizazi 4 vya uzao.
1. ____________ 2. ____________ 3. ____________ 4. ___________

# Je, Muundo Wa Kanisa Letu Wasaidia Au Wazuia Kukua Kwetu?

# MfanoWa Kanisa La Zamani

**Lahusika na washirika na mipango thabiti.**




**Pasipo mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja**
**Mfano huu una nguvu chache za kukua.**

**Huduma kawaida hufanywa kupitia:**

- Ibada
- Ushirika
- Huduma za umri mbali mbali
- Makundi madogo (ukitaka)

**Shida:**

- ni vigumu viongozi kuwafikia watu kwa hivyo mahitaji hayatekelezwi kikamilifu.
- washirika wa zamani hukusanyika pamoja na kuzuia Ushiriki wa watu wapya.
- viongozi wa kutosha hawakuzwi hivyo basi huduma za sasa haziwezi kupanuka na kuzifikia jamii.

**Matokeo:** Kwa sababu mahitaji ya watu hayatekelezwi kupitia kwa huduma mbali mbali, watu huja kwa ibada **kupokea kitu** kuliko **kumwabudu na kumsifu** Bwana.

# Mtindo wa Kale wa Makanisa Umepungukiwa na Uwezo wa Kukua

## Neno la Mungu latwambia:

### 1. Fikia watu - sio kukusanyika pamoja tu

***"............ wanaume kwa wanawake, iliongezeka zaidi na zaidi"***
Matendo ya mitume 5:14.

***"Kama vile Baba alivyonituma mini, nami nawatuma nyinyi".*** Yohana 20:21
Sharti tupange na kujibidisha kuwafikia watu wote wa jamii yetu na injili ya Yesu Kristo.

### 2. Wafundishe watu ili wakomae Kiroho.

***"Kwa sababu hiyo tunamhubiri Kristo kwa watu wote; tunawaonya na kuwafundisha wote kwa hekima yote, ili tuweze kumleta kila mmoja mbele ya Mungu akiwa amekomaa katika kuungana na Kristo. Kwa madhumuni hayo mimi nafanya kazi na kujitahidi nikiitumia nguvu kuu ya Kristo ifanyayo kazi ndani yangu"*** Wakolosai 1:28, 29

Sharti tuwashawishi watu wakue katika Kristo.

### 3. Jenga viongozi

Wadhani Yesu alitumia wakati wake mwingi akiwa na nani, wanafunzi wake au makutano? kwa nini?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Yesu aliwatayarisha wanafunzi wake ili apanue msingi wa uongozi wake.

> "***..Wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza injili, wengine wachungaji na waalimu. Alifanya hivyo apate* kuwatayarisha *watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo*".**
> Waefeso 4:11, 12

**90%** ya viongozi hujengwa kupitia kwa **uhusiano wa Mmoja-Kwa-Mmoja**
**10%** ya viongozi hujengwa kupitia kwa uhusiano wa **Makundi Madogo**.
(Utafiti umefanywa na Al **broom)**
**Ni asilimia (%) ngapi hujengwa katika kusanyiko kubwa? _________**

**Viongozi wa sasa wasipowatayarisha wengine, daima kutakua na upungufu wa viongozi.**


### 4. Kupanua kanisa la Mungu duniani.

Tunapowafikia jamii zetu wenyewe na kujenga wanafunzi na viongozi, yatupasa kuwasaidia wengine wafanye hivyo hivyo katika jamii zao au inchi zao.

# Mfano wa Kanisa Lifanyalo Wanafunzi

## Kundi Dogo/Sherehe

**(Hupenda Ibada na Kuhusika na Washirika)**




## Na Mafundisho ya Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja
## Mfano Huu Una Uwezo wa Kukuza pasipo na Mipaka

**Huduma ina mambo mawili muhimu:**

- Makundi madogo yakuhusiana yanayofanyika nyumbani (4-12)
- Sherehe za jumla (zikiwa kubwa ndio vizuri).

**Faida za huduma ya makundi madogo katika ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja.**

- Washirika hujifunza jinsi ya kutunzana.
- Viongozi waliofundishwa hutoa huduma ya uchungaji kwa kila mmoja.
- Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja hutoa maendeleo ya kiroho
- Makundi madogo huwawezesha washirika wapya kuingia kwa urahisi.
- Waamini wapya huweza kugundua, kukua na kutumia karama zao za kiroho kuhudumu katika makundi yao na kushuhudia Kristo kwa marafiki zao.

**Faida za sherehe za jumla:**

- Sherehe huleta maana kwa makundi madogo.
- huleta furaha katika uimbaji wa sifa, kuhubiri Neno, changamoto ya maono makubwa na nafasi ya shughuli maalum.

**Matokeo:** Mahitaji ya watu hutimizwa wanapokuwa wanafunzi kupitia kwa kundi dogo la Mmoja-kwa-Mmoja. Wataambatana katika roho wa sifa na kumwabudu Mungu. Watafurahi kuwa pamoja na wale wanaowapenda na kuwaleta watu wapya kwa Kristo na kanisani.

# Je, Tunahitaji Kubadilika?

## *Mambo gani yanayopaswa kubadilika?*

**Ni lazima:**

- ☐ tugeuze namna ya kuhudumu ili tuweze kutimiza mahitaji ya watu.
- ☐ **tutilie** mkazo makundi madogo ambako watu wahudumiana.
- ☐ **tutoe** nafasi ili watu binafsi wakue katika mwendo wao na Mungu.
- ☐ **tuachilie** watu wawe na huduma zinazo zaa na kuendelea katika uwezo wa uongozi
- ☐ **tuwafundishe** watu waimarishe mahubiri yenye manufaa kwa wale wanaokaa nao.
- ☐ tuonyeshe umuhimu wa makundi madogo katika ibada na sherehe.
- ☐ tukuze njia nzuri za mahubiri na huduma za mahitaji maalum zitakazo wezesha viongozi wa makundi madogo wawe na ushirika.
- ☐ **tuwaondolee** majukumu mengine wale wanaotaka kuongoza makundi madogo.
- ☐ tuwe na viongozi watakaofanya uamuzi wote kadiri ya vile itakavyowafaidisha viongozi wa makundi madogo pamoja na huduma zao kwa watu wote wanaowatumikia na kuwafundisha.

🗐 ***Weka alama hapo juu ya mambo yale ungetamani yabadilike katika kanisa lako/letu.***

## *Kanisa Litaundwa Namna Gani?*

**Viongozi wa sasa ni sharti:**

- wawe tayari kuchukua hatua nzuri ili watengeneze njia ya ukuaji wa baadaye kwa kuunda kanisa lisilokuwa na vikwazo vya kukua kwa kuzaa viongozi wa sasa.
- wazae viongozi wakutosha watakaowaleta waume kwa wake kwa Kristo na kukomaa katika Kristo katika jamii yetu yote.

# Ili tuwe Kanisa Lenye Nguvu Jinsi Hii, Yatupasa Tugeuke

# Muhtasari

## Kuna njia nyingi za kuwahudumia watu…

1. Sherehe/ibada za **umati.**
2. **Makundi madogo** ya umri mbali mbali.
3. **Makundi madogo** ya watu wasiozidi 12.
4. **Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja** - Mwanaume kwa mwanaume,
   - Mwanamke kwa mwanamke.

## …Bali viongozi hukuzwa katika uhusiano:

1. Asilimia 90% ya viongozi hukuzwa kupitia kwa uhusiano wa **Mmoja-kwa-Mmoja**.
2. Asilimia 10% ya viongozi hukuzwa kupitia kwa uhusiano wa **makundi madogo.**

***Viongozi hukuzwa** kupitia kwa mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja kwasababu:*

1. **Munaweza kukutana wakati wowote**.
2. **Ina kiwango cha juu zaidi**.
3. **Ina nguvu zaidi ya kuongezeka**.
4. **Ina uhusiano zaidi**.
5. **Huleta mfano mzuri wa kuigizwa na mwanafunzi.**

**Viongozi sharti wakuzwe wala sio kuchaguliwa:**

***Eleza mfano wa mtu uliyemfundisha kufanya ile huduma uliyokua ukiifanya wewe:***

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

***Matokeo yake ni nini?***

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**Njia moja bora ya kukuza msingi wa uongozi ni kupitia watu wapya kwa:**

- Kuwafundisha juu ya Misingi
- Kuwasaidia wazae katika mafundisho ya misingi.

# Twawezaje Kukuza Mfululizo wa Kufanya Wanafunzi Katika Kanisa LETU?

# Kustawisha Hali ya Mfululizo wa Kufanya Wanafunzi

# Kukuza Njia ya Kufanya Wanafunzi

***"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;"*** Wafilipi 1: 6

## Kufahamu tofauti ya *mipango* na *mfululizo*:

**Mipango**: Ni sehemu za mfululizo:

**Mfululizo:**

- Una chanzo na huhakikisha ya kuwa mahitaji madogo ya kiroho ya kila mtu yanatekelezwa.

- Ni mpango unaosaidia watu wawe wafuasi waliojitoa kumfuata Yesu Kristo.

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu

**Kumbuka:** ***Fuata mchoro ulioko ukurasa 25 kadri unavyosoma mfululizo huu.***

***Mfululizo huanza tunapo........***

## Shiriki injili na wengine (ona ukurasa 8)

### 1. Jamii:

***Mteja wetu ni nani na watu hawa wa jamii huvutwa namna gani kanisani kwetu?***

____________________________________________________________

### 2. Huduma zinazovutia:

***Huduma zinazovutia sana kanisani kwetu ni gani? (mfano uimbaji, ibada ya kuabudu, vijana, shule ya jumapili, nk.)***

____________________________________________________________

- Huduma hizi ni sehemu ya **viwango vya mvutio na uhusiano**.
  ***Mahitaji ya watu yataanza kutekelezwa namna gani katika viwango hivi?***
- **Wasalimie** na **uwakaribishe** kwa upendo na kuhusika.
- Wanaweza kujifunza kuhusu Kristo kutoka kwa **maandiko** na mfano wetu wa utauwa.


### 3. Kuwatembelea na Kuwafuatia Wageni:

**Wakati mtu anapokuwa na mawasiliano na jamii ya kanisa letu kupitia kwa moja wapo ya huduma hizi, ni hatua gani nyingine tungelifuata?**

❑Kuwapuuza ❑Kuwa uliza wafundishe shule ya jumapili au ❑ tuwajue ili tuweze kuwahudumia.

- Sharti tuwe na lengo la kuwasiliana nao na kumtembelea kila mgeni ili waweze kuelewa jinsi ya kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Mungu.

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu




**Kundi dogo + Mmoja-kwa-Mmoja = Kikundi cha Uhai**

| | | |
|---|---|---|
| ***Shiriki*** *injili na wengine* | *Kuza husiano nao katika makundi madogo na uwafunze katika Misingi katika njia ya kuzaa ili watayarishwe kufunza wengine katika Misingi* | *Viongozi wanaopanua Huduma* |

## Wakristo wapya wakuzwa (Ukurasa 8)

***Mfululizo waendelea ...***

4. **Uhusiano wa Makundi Madogo:**
   ***Tutawaingizaje watu wapya kwenye jamii yetu ya Kristo?***
   - Kila mtu anayetembelewa angealikwa kuhudhuria kikundi kidogo ambapo wangeanzisha uhusiano.

## Wakristo wapya kufundishwa misingi

5. **Uhusiano wa Mmoja-kwa-Mmoja**
   - Uhusiano wa Mmoja-kwa-Mmoja huleta utunzaji wa kibinafsi na kuhusika kunakokuza na kutenda ukweli wa Biblia.

***Mkristo mpya anahitaji nini?***

# Njia Nzuri ya Huduma Itakayowafundisha Watu ili Waweze Kuwa Wanafunzi wa Yesu Kristo Yahitajika

# Hatua Za Kwanza Za Watu Wapya

***Mkristo mpya anahitaji:***

## 6. Ufuataji:

- Wote wanaompokea Kristo wahimizwe ili waweze kuanzisha ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja na watawekwa wawili wawili, mwanaume kwa mwanaume, au mwanamke kwa mwanamke ili waweze kufanya kazi ya ufuataji.

***Wanaendeleaje kukua?***

## 7. Mafundisho ya Ukufunzi

- Baada ya kumaliza kazi ya ufuatiaji watahimizwa kuwa na tabia na maisha ya Ukristo kwa kufundishwa ukufunzi wakiwa na mtu mwingine.

## Uhuru ndani ya Kristo:

**Tambua:** Wanapo gundua wao ni nani ndani ya Kristo wanaweza kutambua kwamba wanadanganywa katika kudhani kuwa wako ndani ya **utumwa wa kiroho**. Watapewa nafasi ya kuhisi ule **uhuru ambao ni wao ndani ya Kristo** wanapoongozwa katika Njia ya **uhuru.**

***Sasa wanapofurahia maisha mapya ndani ya Kristo, watataka kujifunza nini?***

## 8. Mafundisho ya Uinjilisti

- watatamani kujifunza jinsi ya kushiriki imani yao na wengine wanapoendelea na mtu mwingine atakayefundisha juu ya uinjilisti.

Kwa haya yote ni muhimu kuwa na huduma za **Mmoja-kwa-Mmoja** na **Makundi Madogo** kwa maana hapa ndipo ambapo **viongozi hukuzwa.**

**Wafunze katika *misingi* iliwaweze kuzaa katika *misingi!***

# Wanafunzi Wafundishwa Kuzaa **(ukrasa 8)**

## *Mfululizo huu waendelea kwasababu ...*

- Kila mtu aliyepitia mafundisho ya **Uzima Wenye Nguvu** huwa amefundishwa juu ya misingi naye anazo silaha za **kuzaa** katika **misingi**.

- Kuzaa ndio chanzo cha kuwakuza **viongozi**.

- Kukuza viongozi ndicho chanzo cha **kukua** kwa kanisa lenye **kufanya wanafunzi**.

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu Hutayarisha Watu kwa Utumishi

***"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhiwatu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."*** 2 Timotheo 2:2

## Waalimu Wanawafundisha Wengine

***Mfululizo huu unaendelea na kupanuka ...***
Wanafunzi hawa wenye furaha watavutia watu wengine wapya. Kwa maana wamefundishwa na kupewa silaha za kuwahudumia wengine, sasa wataweza kuwa tayari kuwaongoza marafiki zao katika mafundisho ya maisha yenye Nguvu.

# Kukuzwa kwa Kiongozi na Kuingizwa kwa Huduma

### 9. Kukuzwa kwa Kiongozi.

- Kila kiongozi mpya yampasa kuhudumu kama kiongozi mwanafunzi ili kuwatayarisha kwa huduma maalum. Mfano: kiongozi wa kikundi kidogo, kiongozi wa vijana, mabawabu na shule ya jumapili n.k.

- Huenda ukataka kuwafundisha viongozi hawa wapya ili uwafahamishe uongozi wa kanisa letu. Mafundisho haya yangekuwa kama ***kusudi, muundo, ubatizo na ushirika.***

### 10. Kuingia kwa huduma

- Sasa wako tayari kuingizwa katika huduma ambapo wanaweza kuwafikia wengine na injili na kuwafundisha wote wanaompokea Kristo.

## Viongozi Wapanua Huduma

- Viongozi hawa wapya wanaweza kupanua huduma zilizoko au kuanza huduma mpya.

- Kwa maana wamejengwa katika njia ya mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu, watajitolea kuwasaidia wengine.

# Makundi Madogo na Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja Ndizo Njia Nzuri za Kuwafanya Wanafunzi na Viongozi

# Kufahamu Sehemu Mbali Mbali za Mfululizo wa Uzima Wenye Nguvu

Njia ya uzima wenye nguvu ni njia ya hatua kwa hatua ambayo mtu mpya anaweza kuifuata ili akue na kukomaa kiroho katika Kristo. Kila mtu ni tofauti kwa hivyo njia hiyo ni iwe ya kukubalika na mahitaji ya watu wote ifikapo wakati wa mahitaji. Ifuatayo linaeleza sehemu mbili muhimu zinazofanya njia ya kukua, **Uanafunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja** na **Wakati wa Makundi Madogo**.

## Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja

Kila mtu yuko katika kiwango tofauti cha ukomavu wa Kiroho. Kila mtu hupewa nafasi ya kukua kiroho. Mafundisho ya Mmoja kwa Mmoja ni lengo la ukuzi wa kibinafsi utoshelezao unaoweza kukutana na mahitaji yao binafsi. Mwanaume mmoja kwenye kundi hukutana na mwanaume mwengine (au mwanamke kwa mwanamke) kwa wakati wao unaowafaa ( kando ya wakati wa kundi zima) ili wajifunze ukweli wa Biblia pamoja.

***Misingi Yenye Nguvu*** - Masomo 4 yaliyo kusudiwa kuimarisha Mkristo mchanga

***Ukufunzi Wenye Nguvu*** - Masomo 9 yaliyotungwa kuimarisha kuendelea katika maisha ya kiroho.

***Ushirika Wenye Nguvu*** - Masomo 6 yaliyotungwa kwa wale ambao wangetaka kujifunza jinzi ya kuwasiliana vyema juu ya imani yao. Wangepewa nafasi ya kufanya hivyo wanapotembelea watu waliopatikana kupitia kwa kanisa.

***Kila kiwango cha Mmoja-kwa-Mmoja chahitaji kujitoa kwa hali ya juu sana.***
Mafunzo ya Mmoja-kwa-Mmoja hupatikana kwa wote wanaohitaji kukua.

**Uhusiano wa Mmoja-kwa-Mmoja ni Njia Nzuri ya Kuwafanya Wanafunzi na Viongozi Waliohitimu.**

## Kundi Dogo

Madhumuni ya kundi dogo ni **hali ya upendo na kuhusika** ambapo kila mmoja anapata kukua kwenye afya nzuri. Imetungwa isiwe ya kuwatisha watu. Ni pahali rahisi pa furaha kwa wahudhuriaji waletao marafiki. Kiti kisichokaliwa huwakumbusha kuwaombea marafiki na kuwapa moyo wa kuja.


Madhumuni ya muda wa kundi dogo ni:

1. Makaribisho/Ushirika
2. Kuabudu/Maombi
3. Kuvuna Nafsi (Mipangilio ya Uinjilisti)/Maombi
4. Neno – Mafundisho ya Biblia kwa matendo
5. Kukuzwa kwa kiongozi

## Wanao husika kwa Kundi dogo:

(K) Kiongozi
(M) Mwenyeji
(WW) Wakristo Wapya
(WK) Wageni wa kanisa na
(MW) Marafiki wa Wote
(M) Mwanafunzi (kiongozi anaye fundishwa)
(W) Wakristo wa viwango mbalimbali
(W) Wanaotafuta (Wageni walioalikwa)
(K) Kiti kitupu kwa mgeni anayetarajiwa

Kikundi kinaanzilishwa na watu 4 walio tajwa kwa WK, M, K na MK.





Baadaya ya kufundisha watu wachache kwa Maarifa ya Uongozi na Washa za Mafundisho, wanaanza Kikundu/Vikundi cha/vya Uzima cha/vya kwanza.

Katika **Kikundi cha Uhai** kilichochorwa hapo juu kiongozi (K) anamfundisha Mwanafunzi wake (W) kwenye **Ushirika Wenye Nguvu**. Wanapotembelea nyumba ya mgeni wa kanisa (WK) injili inahubiriwa. Kila mtu angealikwa kwenye muda wa kundi Dogo. Kama mtu yeyote angeokoka wakati huo wa matembezi, wangetiwa moyo (Kama Mkristo mpya (MM) kufundishwa juu ya **Misingi Yenye Nguvu**). Wangewekwa wawili wawili katika kundi lile na Mkristo. Wanapomaliza **Misingi Yenye Nguvu**, mtu mwingine pengine mwenyeji (M) angewafundisha kuhusu **Ukufunzi Wenye Nguvu.** Pia wangefundishwa juu ya **Ushirika Wenye Nguvu** na yule kiongozi mwanafunzi ambaye sasa amemaliza mafundisho yake na kiongozi.

# Kundi Dogo Hutoa Maanzilishi ya Huduma.
## Mmoja kwa Mmoja + Kundi Dogo = Kikundi cha Uhai

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu Hutoa Maanzilishi Mema kwa Ukuzi wa Kiongozi




**Ukuzaji wa kiongozi**

## Kundi dogo:

- Kundi linaloanza (Watu 4-6) huenda likawa na mchungaji kiongozi na viongozi muhimu wakiwemo wake/waume wao. Viongozi hawa waweza kuwakilisha huduma mbali mbali kanisani.

## Mmoja-kwa-Mmoja:

- Mchungaji/ kiongozi humfundisha mwanafunzi wake katika ***Kushiriki kwenye Nguvu*** (Mara moja kwa mwezi) **na jinsi ya kuongoza kundi dogo akitumia kujifundisha uongozi na mafundisho ya kiongozi mwanafunzi** **(**Mara moja kwa mwezi).
- Mchungaji huwafundisha wale viongozi wengine kibinafsi au kwenye ***Washa za Misingi Yenye Nguvu*** na ***Ukufunzi wenye nguvu*** kisha nao huwafundisha wengine. Watu hujifunza vyema wanapomuona mwingine akionyesha mfano wa yale wanayotaka kujifunza.

## Ukuzi wa Uongozi ndio Chanzo cha Kuongezeka

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu huzalisha

## Kukua kwa kiongozi


Viongozi na wanafunzi wanapokuzwa, **kundi la kuanzia** huzaa makundi mawili au matatu madogo.

## Kundi Dogo.

- Mchungaji/kiongozi huendelea kuongoza kundi (Kila juma).
- Mwanafunzi sasa ni kiongozi wa kundi lake nao hukutana kila juma.

### Mmoja-kwa-Mmoja

- Kila kiongozi anaye mwanafunzi wake na humfundisha katika ushirika wenye nguvu (Kila mwezi) **na kujifunza kuongoza - mafunzo ya mwanafunzi** (Kila mwezi).
- Washirika waliofundishwa huwafundisha wengine juu ya **Misingi Yenye Nguvu** na **Ukufunzi Wenye Nguvu.** (Hukutana kila juma kando ya mda wa kundi)




Kama viongozi wapya waliofundishwa wanavyokuzwa katika makundi haya mapya, huduma yaweza kupanuka yawe makundi zaidi.

## Kupanuka tuweze kuufikia ulimwengu kwa ajili ya kuzaa.

# Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu Hupanuka


## Kukua kwa Kiongozi

## Kundi dogo (La viongozi)

- Mchungaji akiwa mwalimu wao hukutana kila mwezi na kundi lake la viongozi kwa ajili ya maono, ufahamu, kusuluhisha shida, maombi na mafundisho wakitumia mafundisho ya **V*iongozi Wanaoongoza.***

## Mmoja kwa Mmoja:

- Kila kiongozi humfundisha mwanafunzi wake **kibinafsi** katika ***Ushirika Wenye Nguvu*** kila mwezi) na pia hukutana kwa kutiana moyo, maombi na kujifunza jinsi ya kuongoza kundi hili dogo kupitia kwa ***kujifunza kuongoza - mafunzo ya wanafunzi***(Mara moja kwa mwezi).
- Washirika waliofundishwa huwafundisha wengine juu ya **Misingi Yenye Nguvu** na **Ukufunzi Wenye Nguvu.** (Hukutana kila juma kando ya mda wa kundi)




Viongozi wanaozaa kwa kuwaleta na kuwafundisha wanafunzi wao ili wawe viongozi wapya wanaweza kuendelea kuwafundisha viongozi hawa wapya.

# Mwongezeko ndio Kanuni ya Mungu ya Kuufikia Ulimwengu

# Uweza wa Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu


## Kukua kwa Kiongozi

## Kundi Dogo (la Waalimu)

Mchungaji anaendelea kukutana kila mara na waalimu kwa maono na mipangilio.
Waalimu hukutana na viongozi kwa kutoa ripoti, kusuluhisha matatizo, maombi na mafundisho ya ***kujifunza kuongoza - kuwafundisha viongozi***.

## Mmoja-kwa-Mmoja:

- Kila kiongozi humfundisha mwanafunzi wake kibinafsi juu ya ***Ushirika Wenye Nguvu*** (kila mwezi) na pia hukutana kwa kutiana moyo, maombi na mafundisho juu ya kuongoza kundi dogo wakitumia ***Kujifunza Kuongoza - Mafunzo yo Kiongozi Anayejifunza*** (kila mwezi).
- Washirika waliofundishwa huwafundisha wengine juu ya **Misingi Yenye Nguvu** na **Ukufunzi Wenye Nguvu.** (Hukutana kila juma kando ya mda wa kundi)





Mchungaji anapowafundisha viongozi wa huduma mbali mbali za kanisa, watatekeleza njia ya **Mfululizo wa Maisha Yenye Nguvu** katika huduma zao.

# Mpangilio wa Uongozi usio na Mipaka ya Kukua

# Kanisa Lenye Kufanya Wanafunzi

## Uzao Unafanyika Katika Kila Huduma ya Kanisa




**Makundi Hupanuka na Kuongezeka ili Hatimaye Kuwe na Wanafunzi wa Kutosha wa Kushuhudia Kuweza Kuufikia Ulimwengu!**

# Muhtasari

## Mfululizo wa Kufanya Wanafunzi

### Shirikiana Injili ya Yesu Kristo na Wengine

- Kanisa **hukua** kwa sababu huwafikia na **kuvuta** watu wengi zaidi.

### Wafundishe Wakristo Wapya Misingi ya Maisha ya Ukristo

- Watu hujifunza **kuwa wanafunzi**

### Kutayarishwa Kuzaa

- Watu hutayarishwa **kuzaa**
- Watu hujifunza **kufanya wafuasi**
- Watu hujifunza **kuongoza kundi dogo**

### Ukuzi wa Kiongozi na Huduma Yake.

- Viongozi hukuzwa **unapoendelea** kukusanya watu zaidi na **kuwapa mafundisho** zaidi na **kuwatayarisha.**
- Viongozi wa makundi madogo hujifunza kuzaa viongozi wengine na kuanzisha kundi lengine.
- Viongozi wa makundi madogo hujifunza **kuwakuza viongozi wanafunzi**
- Washirika hujifunza **kukaribisha** na **kuwafundisha** watu wapya.
- Huduma za kanisani huanza kutekeleza **lengo la ukufunzi** wa Mmoja-kwa-Mmoja.
- Viongozi wa kanisa **hutekeleza** na **kuunganisha** maono ya huduma ya makundi madogo kama njia ya **msingi** bora wa kuvutia wafuasi na kutunza watu wapya.
- Viongozi wenye bidii hujifunza jinsi ya **kuwafundisha** na **kuwalea** viongozi wengine.
- **Mafundisho** zaidi ya **ustadi** hufanywa kwa ukuzi wa viongozi
- Umuhimu wa uongozi wa kanisa ni kusaidia viongozi wa makundi madogo **wafaulu** kwa kusaidiwa na kufundishwa.

## ***Mungu Akubariki Unapoongoza Kanisa Lako Kwenye Maisha Yajayo Yenye Nguvu!***

# Namna ya Kuanza

## Washa za Kukuza Mfumo wa Maisha Yenye Nguvu

*"Kuongoza Kanisa Kwenye Maisha Yajayo ya Nguvu"*

# Washa za Mazoezi Kwa Kundi Lako la Kuanzia


**(Saa 1-1 1/2)**

Kwa sababu sasa umemaliza vipindi vya ***Mipangilio ya Uongozi*** na unaelewa umuhimu wa kuwa na ***Mfumo wa maisha yenye Nguvu*** na jinsi ya kuwa kanisa lenye kuleta wafuasi, ni muhimu ya kuwa uanze vyema. Washa hii itakupa ujuzi na ujasiri ***unapoanzisha kundi lako.***

**Kuna Nini Katika Jina?**

Huenda ikawa tayari una kundi dogo au huduma ndogo. Kama haina viungo sawa vya ufuasi wa Mmoja-kwa-Mmoja na ukuzi wa uongozi nawe waamini kuwa hizi ndizo kanuni unazotaka kuziingiza ndani, utahitajika kuchagua jina tofauti la kundi lako jipya. **Jina likiwa moja, akili haitaweza kubadilika.** Unaweza kutumia jina lolote unalotaka lakini hebu zingatia maoni yafuatayo:

Neno ***Kikundi cha Uhai*** huwakilisha kanuni kamilifu za ***Njia Yenye Uhai wa Nguvu***, mfano:




**Mmoja kwa Mmoja + Kundi Dogo = Kikundi cha Uhai**

Katika Washa hii tutaona muda wa **Kundi Dogo** wa ***Kikundi cha Uhai***. Pia utahitajika kuwafundisha washirika na viongozi kwenye mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja.

**Ujuzi wa Kundi Dogo**
Chagua viongozi waliojifunza vipindi vya filosofia/lengo na waliotayari kushiriki kwenye ***kundi linaloanza.*** (Waweza kuanza na makundi kadhaa kama una viongozi wakutosha wenye bidii).

Chagua viongozi 4-6 wafuatao kwa kila kundi linaloanza:

Kiongozi (Mchungaji au Kiongozi mdogo) ________________________________________

Mwanafunzi (Kiongozi anayejifunza) ____________________________________________

Mwenyeji (Karama ya ukarimu) _________________________________________________

Wakristo waliokomaa (viongozi wazuri) ____________________________________________

Ongezea Wakristo Wapya au wasioWakristo kwenye makundi/kundi yako/lako ya /la kuanzia

**Kumbuka:** ***Mchungaji/kiongozi unda makundi ya watu 4 au 6. Weka kila kundi uhuru wa kuchagua kiongozi wao. Kiongozi naye achague msaidizi wake au mwenyeji. Wape viongozi wako majukumu yafuatayo kisha uwaongoze unapofuatilia lengo la makundi madogo yaliyoelezwa hapo chini ili waweze kuelewa mambo utakayofanya katika mikutano ya kila juma. Furahieni kukutana kwenu pamoja.***

## Lengo La Kundi Dogo

# Makaribisho (Dakika 15-20)

**Mwenyeji**
- Panga viti katika mzunguko wa karibu, ukiongeza kiti kimoja peke yake.
- Wasalimie kila mtu kwa njia ya upole
- Nakili jina la kila mtu aliyehudhuria ukitumia **nakala ya waliofika** ifuatayo

**Kiongozi**
- Fungua Kwa maombi au umuulize mtu mwingine aombe.

**Msaidizi** (kiongozi anayejifundisha)
- Ongoza kipindi cha ushuhuda (toa dakika15-20)
  Tumia maswali ya ushuhuda yafuatayo. Chagua swali moja kisha utoe nafasi kwa kila mtu atoe jibu au wanaweza kushiriki jambo zuri au baya katika juma lao au wanaweza kumpisha mtu mwingine kama jambo la kushiriki.
- Toa nafasi kwa mtu mmoja au wawili ili watoe ushuhuda wao wa dakika moja.
- Zungumza wazi na ukweli.

# Kuabudu ( dakika 15-20)

**Kiongozi**
- **Ongoza kwa wimbo/nyimbo za sifa au ibada.**
- **Mshukuru Mungu kwa maombi aliyojibu.**
- **Mtukuze Mungu kwa wema wake.**
- **Shiriki meza ya Bwana ikiwezekana.**
- Wape moyo ili kila mmoja ahusike. Musiombe mukifuatia mzunguko wala usihaibishe mtu yeyote.

# Shawishi (Dakika 20-30)

**Msaidizi(kiongozi anayejifunza)**

- Chunguza maendeleo ya washiriki wa Mmoja-kwa-Mmoja katika Misingi, Ukufunzi au Ushiriki
- Chunguza au tambua wale walio tayari kufundishwa au kufundisha wengine.
- Fanya mipango na matayarisho au uinjilisti.
- Toa Muktasari kuhusu mipangilio ya maombi ya wokovu katika eneo lako.
- Ongoza Kipindi cha maombi. Omba ya kwamba mtu atakuja kukalia kile kiti kitupu wakati ujao. Mjizoeze kuomba maombi mafupi(maombi ya sentensi fupi). Letene hoja zenu ili ziombewe. Wengine wanaweza kuungana nawe kuombea hoja hizo au hoja zinginezo.
- Nakili hoja zenu na majibu ya maombi yenu katika nakala ya Maombi Zaidi-Nguvu-Zaidi-Sifa Zaidi

# Neno (Dakika 20-30)

**Kiongozi**

- Ongoza **Kipindi cha mafundisho ya Biblia**.
- Tumia mifano ya **masomo ya uzima** ifuatayo katika kitabu chako cha mafundisho.
- Kumbuka ya kuwa **hupaswi kufundisha au kuhubiri** bali ni uongoze mazungumzo ya wale washirika.
- Funga ushirika - fanya matangazo yoyote.
- Watie moyo ili kila mtu arudi na alete rafiki mpya ni Mkristo au sio Mkristo.
- **Tawanya** kikundi kwa **maombi**

## *Washa ya Mazoezi Kwa Kundi Lako la Kuanzia!*

**Mwenyeji**

- Vinywaji (sio lazima)
- Ikibidi uandalie vinywaji, basi visiwe vya gharama

**Leo kabla ya kutawanyika, mkamilishe daftari ya mpangilio hapo chini**

**=====================================================**

### Mchungaji/Kiongozi ongoza wakati wa mazungumzo na mpangilio ufuatao

1. Pata ahadi kutoka kwa kila mmoja aliye tayari kuhusika katika kundi linaloanza.

2. Mthibishe Mkufunzi wako_____________________________________________

3. Mthibitishe Mwenyeji __________________________________________________

4.Thibitisha mambo yafuatayo: Siku _________ Tarehe ya kuanzia ________________

Wakati wa Kuanza ________ Wakati wa kufunga ______________

5. Chagua jina la Huduma ya kundi lako Dogo. Ona *Kuna nini katika jina* hapo juu

6. Chagua taratibu za mda wa mafundisho ya Biblia kwa kikundi chako. Ungependa kuanza na *Masomo ya Uzima* yenye sehemu 24. Kuna masomo mengine unayoweza kuchagua. Ona *kuchagua taratibu kwa ajili ya makundi yako* yanayofuata.

7. Chagua wakati wa kukutana na mwanafunzi wako mpitie sehemu za *Kujifunza Kuongoza – Kiongozi Mwanafunzi* ( mara moja kwa mwezi kwa lisaa moja). Pia chagua wakati ukague *Kushiriki Kwenye Nguvu* ( mara moja kwa mwezi kwa masaa 2).

   Vipindi vya ***Kujifunza Kuongoza*** : Tarehe ________ Wakati _______ Pahali __________

   ***Ukufunzi Wenye Nguvu***: Tarehe ____________Wakati _________ Pahali ____________

## Mafundisho Ya Ufuasi ya Mmoja-kwa-Mmoja

**Chaguo la 1:** Chagua wakati wako na wa mkeo au mwanamke mwingine aliyekomaa ili muanze kuwafundisha viongozi wengine (Wanaume kwa wanawake) katika Mmoja kwa Mmoja.

**Misingi Yenye Nguvu:**

Nitafundisha __________________________ (mwanaume hufundisha mwanaume)

_____________________ atamfundisha _____________________(Mwanamke hufundisha mwanamke).

Kila mmoja wetu atamfundisha mtu mwingine atakayemfundisha mtu mwingine n.k.

==================================================================

**Ukufunzi Wenye Nguvu:**

Nitamfundisha _________________________ (Mwanaume hufundisha mwanaume)

_______________________ atamfundisha ______________________(Mwanamke humfundisha mwanamke).

Kila mmoja wetu atamfundisha mtu mwingine atakayemfundisha mtu mwingine n.k.

==================================================================

**Chaguo la 2:** Weka siku za washa 2 za Mmoja-kwa-Mmoja ***Misingi Yenye Nguvu*** (saa 1 ½ ) na nusu)na ***Ukufunzi Wenye Nguvu*** (saa 1 ½ Lisaa limoja na nusu). Viongozi wanaweza kufundishana baada ya washa.

**Washa za Misingi Yenye Nguvu (saa 1 ½)**

Tarehe ________________________ saa _____________________ Pahali _________

Baada ya washa _____________________________ atamfundisha ________________

Baada ya washa _____________________________ atamfundisha ________________

Baada ya washa _____________________________ atamfundisha ________________

**Washa ya Ufuasi Wenye Nguvu (saa 1 ½)**

Tarehe ____________________ saa ______________________ Pahali ______________

Baada ya Washa ______________________________ atamfundisha ________________

Baada ya Washa ______________________________ atamfundisha ________________

Baada ya Washa ______________________________ atamfundisha ________________

==================================================================

**Washa ya Kushirika Kwenye Nguvu (saa 2)**

Viongozi watawafundisha viongozi wanafunzi kibinafsi kwenye ***Ushirika Wenye Nguvu***. Huenda ukataka kufanya ***Washa ya Kushirika WenyeNguvu*** kudhihirisha matembezi ya nyumbani. Hii inaweza kuondoa hofu ya wale walio na woga wa uinjilisti wanapoona matokeo mazuri ya matembezi haya. Watafurahia kujifunza namna ya kushuhudia imani yao. Shirikiana furaha yako. Shiriki kumpongeza kila kiongozi. Funga kwa maombi.

## Kundi La Uzima

### Nakala Ya Mahudhurio Ya Kila Juma

| **Jina La Mwisho,** ***Mume*** ***Mke*** | Tarehe | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | |

# Maswali ya Kushirikiana

Shirikiana moja wapo ya siku zako za furaha maishani mwako.
Utajielezaje wewe mwenyewe kwa mtu mwingine asiyekujua?
Ni rangi gani inayoeleza hisia zako leo?
Nini inatupendeza zaidi katika maisha ya rafiki yako?
Ni njia gani isiyo ya kawaida ambayo Mungu amenena nawe?
Ni kitabu gani kizuri ambacho umewahi kukisoma? Kwa nini?
Kama kungekuwa na kitu ambacho ungetaka kibandikwe katika kaburi lako unapokufa, kingekuwa kitu gani?
Ni kazi gani unayofurahia kufanya ukiwa nyumbani?
Ni zawadi gani nzuri zaidi uliyoipata? Kwa nini?
Kama ungeweza kugeuza kitu kimoja katika maisha yako, kingekuwa nini?
Ni lini ambapo Mungu alikuwa zaidi ya neno kwako?
Shiriki mahali ulipoishi na kitu kimoja chakukumbuka ulipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili.
Ulipokuwa unakuwa, ni mchezo gani uliofurahia kucheza.
Ni aina gani mbili au tatu za urithi ulizonazo? Kwa nini ni za thamani?
Ni kitu gani unachotamani kupata katika maisha yajayo?
Ni uhusiano gani wa binafsi unaotamani kuufanyia kazi?
Ni lini uliposikia habari za Yesu kwa mara ya kwanza na ulifikiri nini juu yake?
Eleza maisha yako leo kuhusiana na maelezo ya hali ya anga.
Ni kitu gani kinachokutosheleza maishani mwako?
Jambo la kuogofya zaidi lililonipata ni.
Ningependa kusafiri kwenda.
Unapokuwa na wakati wa uhuru, unapenda kufanya nini?
Katika nyumba yako, ni sehemu gani unayoifurahia zaidi na ni kwa nini?
Je umewahi kuwa na mnyama aliyekufurahisha ukiwa mtoto wako? Kwanini alikuwa wa maalumu?
Ni mabadiliko gani ambayo ungependa kuyaona wakati wa mapumziko yako wakati kama huu mwakani.?
Ni mtu gani (Mbali na Kristo) ambaye anagusa maisha yako. Kwanini?
Ni nani aliyekuwa rafiki yako wa karibu ulipokuwa unakuwa. Kwanini?
Sikuweza kushikilia sana____________________
Mwaka huu ujao waonekana mzuri kwangu kwa sababu _________________
Watu wanaweza kushangaa wanapojua ya kuwa mimi ni ______________
Unafanya nini mwisho wa siku au juma ili kuondoa uchovu?
Ni kitu gani kinachokutisha? Kwa nini?
Ni manutano gani mazuri yanayokupendeza na ni ukumbusho gani unayoyaambatanisha nayo.

# *Mafundisho ya Uhai*

**MWITO WA WANAFUNZI WA KWANZA**
**LUKA 5:1-11**

Jibu swali, **"Je ulisikiaje wakati wa kwanza ulipo ..."**

1. jaribu kuogelea  2. jaribu mchezo mpya  3. kosa kwenda shuleni
4. ondoka nyumbani kwenu  5. pata kazi

================================================================================

**KUKUTANA NA MAANDIKO**
Soma Luka 5:1-11 kisha ujadili

***1.*** Je unafikiri ya kuwa ilikuwa ni bahati tu ya kuwa Simoni Petro ***alikuwa "akiziosha nyavu zake"*** wakat Yesu alipohitaji dau.... au ulikuwa mpango wa Mungu?
a. ni bahati tu  b. Mpango wa Mungu  c. sina uhakika

***2.*** Kama wewe ungekuwa Simoni Petro wakati Yesu alipomuuliza ***"kuzama kilindini na ashushe nyavu zake ili apate samaki wengi,"*** wewe ungeliitikiaje?
a. kama Petro alivyofanya  b. Ningetoa sababu ili nisifanye
c. ningemtia Yesu moyo aendelee na mahubiri yake na mimi nivue samaki.
d. Ningetoa maoni ya wakati mwingine ambao samaki ni wengi
e. Ningeendelea kuvua kwa manung'uniko

3. ***"Walipovua samaki wengi namna hii mpaka nyavu zao zilipoanza kukatika"*** unafikiria Simoni Petro alikuwa anafikiria nini?
a. juu ya pesa zote angepata kwa samaki hawa wengi  b. jinsi alivyokosea kumshukuru Yesu
c. Hakujua la kufikiria  d Alitambua Yesu ni nani

4. Wakati Simoni Petro aliposema, ***"Niondokee, Bwana, mimi ni mwenye dhambi!"*** alimaanisha nini?
a. Nimenyenyekea kwa sababu wewe una ujuzi zaidi wa uvuvi kunishinda
b. Siwezi kukaa nawe kwa ajili ya dhambi zangu
c. Ninatambua kwamba wewe uko vile usemavyo uko, lakini mimi siko tayari kukufuata.
d. Koma kunifanya nijione na hatia. Niache kabisa
e. Nimechanganyikiwa. Ninataka kukufuata wewe lakini nikisema "ndio", najua kwamba itabidi maisha yangu yabadilike nami naogopa.

================================================================================

**MATUMIZI**
Zingatia safari yako ya kiroho.

1. Je mwanzo wako wa kiroho unaweza kulinganishwaje na ule wa Simoni Petro.
a. sio wa vichekesho kama wake  b. wa kielimu zaidi  c. wa kutatanisha
d. wa vichekesho zaidi  e. tofauti, lakini ni ya ukweli  f. sina uhakika

2. Je ungeelezaje hali ya dau lako la kiroho?
a. yazama  b. imekwama  c. yaenda mrama  d. yahitaji kurekebishwa
e. yaelekea sawa sawa  f. imepigwa na dhoruba nyingi

3. Kama Yesu angekuuliza ***"zama kilindini kisha ushushe nyavu zako upate samaki wengi"***, ungeliitikiaje?
a. ningeogopa  d. Nitafanya kama mwingine atavngana nami
b. Ningefikiria kuwa jambo la ujinga  e. vyema! tutaanza lini?
c. sawa, lakini....  f. sikuelewi

4. Ni kitu gani kingekufanya wewe uendelee?
a. wakati wa kuhesabu gharama  b. wakati wa kujipanga  c. sina uhakika
d. msaada kutoka kwa marafiki  e. msaada wa kusafisha maisha yangu  f. utiifu

**MAOMBI MENGI -**
**NGUVU NYINGI -**
**KUSIFU KWINGI!**

| MAAGIZO | Tarehe | JIBU | Tarehe |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

# Kuchagua Taratibu za Makundi Yenu

Himizo lapaswa kuwa katika **matumizi** kwasababu lawama ya mshirika wa kanisa la leo ni nia ya **kupokea,** kutafuta ufahamu zaidi; na **utoaji** ni mchache sana, utiifu wa Kristo katika sehemu za ushuhuda kwa wengine ni haba mno. Ndiposa mafundisho ya Biblia yapaswa kutimiza nia ya matumizi, utiifu na matendo.

**Maswali ya kuzingatia katika kuchagua taratibu**

Lengo letu ni nini?
Mahitaji muhimu ya kundi letu wakati huu ni nini?
Kundi letu lime komaa namna gani kiroho?
Linafaida gani katika kanisa letu?
Je, linatoshea katika mda wa dakika 20-30?

Taratibu za mafundisho ya Biblia yaweza kuwa **juu ya ujumbe**, lakini **himizo lazima liwe katika matumizi**. Mchungaji anaweza kutayarisha muhtasari wa ujumbe kisha awaonyeshe watu wote katika ibada. Pia yeye au mtu mwengine anaweza kuandaa maswali ya kutumiwa katika makundi madogo yanayoongoza kwenye matumizi. Viongozi pia wanaweza kusaidia kutunga maswali haya.

Taratibu itakayofuata yaweza kuwa na mafundisho ya Biblia kuhusu mambo fulani au mafundisho mengine yaliyotungwa kwa ajili ya makundi madogo kama: ***Mafundisho ya Uzima*** kutoka kwa Dynamic Churches International (ona mfano) na mafundisho ya Serendipity.

Hakikisha ya kuwa taratibu ni ya **manufaa ya kundi** lote ukiruhusu kuhusika kwa wote. Maswali matano au sita mazuri yakiandamana na matumizi huwa yanatosha. Ni lazima yawe ni maswali ya **kwa nini** wala sio maswali ya **nini**.

Kumbuka ya kuwa washirika wengine wa kundi watahusika katika mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja na waalimu wao. Kusiwe na matayarisho yoyote kabla ya kundi kukutana. Hii yaweza kumvunja moyo mtu mwingine asije kwenye kundi kama hajamaliza kazi aliyopewa. Pia kila somo lapaswa kuwa peke yake (sio mfulizo wa mafundisho yaliyopita) kwa sababu itakuwa vigumu kwa mtu mgeni kuanzia katikati ya mfululizo huu wa mafundisho.

# Maagizo Ya Waalimu wa Washa

***Kumbuka: Mchungaji/kiongozi anaweza kuanza kwa kuwafundisha mtu mmoja kwa mmoja misingi yenye nguvu na ukufunzi wenye nguvu. Kila mtu aliyefundishwa anaweza kuwafundisha wengine ambao nao watawafundisha wengine n.k. Anaweza pia kutumia njia hii ya washa kuwaeleza watu wengi zaidi ambao wangeambatana wawili wawili na kumaliza mafundisho baada ya Washa.***

## Washa ya Misingi yenye Nguvu (saa 1 ½)

- **fungua kwa maombi**
- hakikisha kuwa kila mtu yuko na nakala ya ***Misingi yenye Nguvu*** **ambayo ina mwongozo wa viongozi.**
- wasaidie kupata mwongozo wa viongozi**.**
- soma mwongozo wa viongozi kisha chambua mambo kama ***Nafasi ya Ukufunzi wenye Nguvu*** (ukurasa wa 17) na ***Hati ya Kufaulu*** itolewe baada ya kumaliza mafunzo ya Misingi yenye nguvu na mmoja kwa mmoja.
- chagua mshiriki mmoja **umtumie** ukipitia sehemu ya kwanza ya ***Misingi ya Nguvu*****:**
    - Jitambulisheni
    - Ongoza kwenye sehemu ya kwanza
    - Jadili alama ya kwanza na ya pili
    - wasaidie wengine waungane wawili wawili (mwanamke kwa mwanamke, na mwanaume kwa mwanaume)

***Kumbuka: Wakufunzi muwe tayari kuungana wawili wawili na mshiriki kama inavyohitajika au uwe na watu 3 wakifanya kazi pamoja.***

- wakiwa wawili wawili waache waamue wenyewe ni nani kati yao atakayechukua nafasi ya Mkristo mpya na ni nani atakayekuwa mkufunzi.
- waache waendelee mahali ulipowaachia na wamalize sehemu ya kwanza wakianza alama ya 3)
- uwe tayari kuwasaidia au kujibu maswali wanapofanya sehemu ya kwanza.
- wanapomaliza angalia majibu yao ya sehemu ya kwanza kuwahakikishia ya kuwa wameimaliza sawa sawa.
- **wape nafasi ya kuuliza maswali sasa**
- waache waendelee na sehemu ya pili wakati unaporuhusu
- wape nafasi ya kupanga siku na wakati wa kukutana na wale walioungana nao ili wamalize sehemu zote 4 katika majuma yafuatayo baada ya washa ya mafundisho. Washiriki wote sharti wawe tayari kuwafuata wakristo wapya au wawafundishe wakristo wengine waliokomaa hata kabla ya kumaliza sehemu zote 4 wakiwa na washiriki wao.
- waache wawe na wakati wa maombi pamoja, kisha **funga kwa maombi.**

**Washa ya Misingi yenye Nguvu**

Tarehe ________________ Wakati________________ Mahali ____________
Baada ya Washa __________________ atafundisha _________________________
Baada ya Washa __________________ atafundisha _________________________
Baada ya Washa __________________ atafundisha ________________________

# **Maagizo ya Wakufunzi wa Washa** (yaendelea)
# **Washa ya Ukufunzi wenye Nguvu ( saa 1 ½ )**

- **fungua kwa maombi**
- hakikisha ya kuwa kila mmoja anayo nakala ya ***Ukufunzi wenye Nguvu*** ambayo ina ***Maagizo jumla ya Wakufunzi***. Wasaidie waweze kuyaona maagizo ya mwalimu baada ya ***Ukufunzi wenye Nguvu.***
- soma maagizo ya jumla bila kusema kitu.
- waweke wawili wawili (mwanaume kwa mwanaume, na mwanamke kwa mwanamke) kisha waache wenyewe waamue ni nani kati yao atakayekuwa mwalimu.

***Kumbuka: Waeleze ya kuwa ni kawaida unapofanya kazi ya uanafunzi ya kwamba kunge kuwa na mwalimu ambaye angekuwa amekamilisha masomo yote kabla ya mkutano kuanza, na mwanafunzi anayesoma masomo yote kwa mara ya kwanza. Leo mwalimu hakumaliza somo peke yake. Wote watakuwa wakisoma pamoja. Amueni ni nani atakayekuwa mwalimu.***

- waambie wafungue ukurasa wa kwanza. ***Angalia somo la kwanza*** kisha ufuate orodha hii. Angalia kila kazi mnapoimaliza kwa pamoja. Fanyeni kadri muwezavyo katika wakati tulio nao.
- waambie wamalize somo la kwanza katika ***Kumjua Yesu kama Mwokozi Wangu*** mkianzia ukurasa wa kwanza.
- uwe tayari kujibu maswali yoyote unapozunguka na kutazama. Hakikisha kila mmoja yuko na mwenzake na wafanye **Somo la Kwanza.**
- muda unapoisha, walete pamoja tena. Jadilianeni baadhi ya maswali yao ili wajisikie na ujasiri utakao wawezesha kuwafunza wengine.
- **toa nafasi ya maswali sasa.**
- angalia ***Somo la Pili - Maandalizi Yafanywe*** kabla ya kukutana wakati mwingine.
- wape nafasi ya kupanga siku na wakati watakaokutana na washirika wao ili wamalize masomo yaliyobaki kwa majuma yajayo. Washirika wote sharti wawe tayari kuwafundisha wakristo wapya ama wakristo waliokomaa hata kabla ya kumaliza masomo yote 8 na washirika wao.
- **funga kwa maombi**

**Washa ya Ukufunzi wenye Nguvu (saa 1½)**

Tarehe ________________ Saa _____________ Mahali _________________

Baada ya Washa ______________________ atafundisha ___________________________

Baaday ya Washa_____________________ atafundisha ___________________________

Baada ya Washa______________________ atafundisha ___________________________

# Maagizo ya Wakufunzi wa Washa (yaendelea)
# Washa yak Ushiriki Kwenye Nguvu (Masaa 2)

***Kumbuka: Kila mshirika sharti awe na kitabu cha ushirika wenye nguvu kisha akamilishe somo la kwanza kabla kuja kwa washa. Hili ndilo taraja la somo la kwanza ushirika la wenye nguvu.***

- **Fungua kwa maombi.**
- Hakikisha ya kuwa kila mmoja yuko na nakala ya Ushiriki wa nguvu pamoja na maagizo ya jumla ya wakufunzi. Wasaidie kuyaona mnapofika mwisho wa ***Ushirika Wenye Nguvu***.
- Soma maagizo ya jumla bila kusema kitu chochote (Maagizo mengine ni sawa na yale ya ***Ukufunzi Wenye Nguvu***).
- Sharti kila mmoja awe amekamilisha ***Somo la Kwanza*** la ***Ukufunzi Wenye Nguvu***. Kami washiriki hawajamaliza kufanya somo la kwanza itabidi kuwapa mda zaidi ili waweze kukamilisha somo hili wao wenyewe. Kisha uendelee.
- Sharti kila mmoja awe amemaliza somo la swanza. Angalia jinsi walivyomaliza somo la kwanza.
- Uwe tayari kujibu maswali unapozunguka na kuangalia.
- Walete tena pamoja. **Wape nafasi ya kuuliza maswali.**
- Waulize kama kuna yeyote aliye tayari kutoa ushuhuda wa dakika moja. Waruhusu baadhi yao washuhudie kama kuna wakati mzuri.
- Hakikisha kuwapa moyo na kuwapongeza wote waliotoa ushuhuda.
- Baada ya kila mmoja kushuhudia uliza kundi kutambua baina ya awali, jinsi gani na baadaye ya ushuhuda wao. Kwa utaratibu gundua sehemu zinazohitaji kukuzwa.
  **Uwe mwangalifu ili usimwaibishe mtu yeyote**.
- **Ngojea ili mtu mmoja achague maonyesho ya matembezi ya nyumbani**.

## Mapumziko (Dakika 15)

### Wakati wa mapumziko tayarisha maonyesho ya matembezi ya nyumbani.

- Hakikisha kujitayarisha kabla ya wakati.
- Chagua mshirika mmoja mtakayekuwa pamoja katika maonyesho hayo (Mtu aliyetoa ushuhuda mzuri sana wa dakika moja). Muombe awe mshirika wako. Itampasa akuangalie wewe na atoe ushuhuda wake unapomuita.
- Chagua jamii moja kati ya kundi ili wafanye kazi ya jamii ambayo ungeitembelea.
- Waagize wale utakaowatembelea waitikie jinsi wangelifanya wakati sio Wakristo walioisikia injili na wako tayari kumpokea Kristo. Ni sharti pia waitikie Mwito wa kuhudhuria mafundisho ya uhai na ***Misingi Yenye Nguvu***.
- Andaa meza ndogo na viti 4 kwenye meza hiyo (mtu yeyote asielekeze mgongo wake kwa kikundi)

# Anza maonyesho ya matembezi (Dakika 30)

- Eleza kundi lote yale utakayofanya kisha uwaambie wafuatane na matembezi yako ukianzia kwenye alama ya **C**. Kanuni za kuwasili katika somo la tatu la ***Ushiriki wa Nguvu***.
- Kila mtu mpe vitabu vya ***Je ungependa kumjua Mungu wewe binafsi?*** au ***Je Umewahi Kusikia Kuhusu Kanuni nne za Kiroho?*** Waambie wasome nawe unaposoma kitabu pamoja na ile jamii kwenye maonyesho ya matembezi.
- Watambulishe mshirika wako na jamii mutakayoitembelea.
- Wakaribishe kwenye meza ile jamii utakayoitembelea.
- Wewe na mshirika wako mjifanye mnakuja kwa mlango wao. Wamkaribishe na kumuuliza mje mezani.
- Fuateni mtindo wa matembezi ulioelezwa mkianzia kwenye **C**. Kanuni za kuwasili iliyoelezwa katika somo la tatu la ushirika wenye nguvu.

***Kumbuka:* Hakikisha unasoma kitabu cha injili bila kutoa maelezo yeyote. Ni muhimu kwamba ufanye mfano mzuri.**

- Baada ya maonyesho ya matembezi washukuru wote waliohusika.
- Toa nafasi ya maswali katika ushirika wenye nguvu au yale matembezi.
- Eleza ya kuwa viongozi watawafundisha wanafunzi wao juu ya ushuhuda wa nguvu lakini kila mmoja anakaribishwa kufundishwa.
- Watie moyo kila mmoja ashiriki na mwingine juma hili juu ya kitabu cha injili. Wakumbushe ni rahisi kuifanya na inafaida sana.
- **Funga kwa maombi.**

**Washa ya ushirika wenye nguvu (Masaa 2)**

Tarehe ______________________ Saa __________________Pahali_______________

Baada ya washa _______________________ atamfundisha ______________________________

Baada ya washa _______________________ atamfundisha ______________________________

Baada ya washa _______________________ atamfundisha ______________________________

**Hati ya kujitoa** ya kiongozi wa kundi la uhai iliyopo katika ukrasa ufuatao sharti ijazwe na wale waombao kuwa viongozi wa makundi.
**Hati ya kufaulu** ni sharti ijazwe na kuwekwa sahihi na mkufunzi kwa wote waliomaliza mafundisho haya.

## Hati ya Kujitoa ya Kiongozi wa Kundi la Uhai

Mimi ______________________________, najitoa kwa Mungu, ili nimtumikie Kristo na kanisa lake.
Nitajitahidi kutoa uongozi wa utumishi kwa wote walio mikononi mwangu na kuufikia ulimwengu katika upendo.

Anwani ________________________________________________________________

_________________________ Nambari ya Simu ____________________

Ninapowekewa mkono wa kuwa kiongozi wa kanisa letu, naahidi:

_____________ Kuomba kila siku.

_____________ Kuishi maisha ya Kibiblia kwa imani.

_____________ Kumruhusu Roho Mtakatifu ayaongoze maisha yangu.

_____________ Kutoa kwa ajili ya kazi ya Mungu.

_____________ Kuwa mwaminifu kwa kanisa na viongozi wake.

_____________ Kuhudhuria mikutano ya viongozi na mafundisho.

# ***Cheti cha Kuhitimu***

**Hii ni kuthibitisha kwamba**

_________________________________________________________________

**amefaulu kukamilisha**

***Washa za Maarifa na Mafundisho ya Uongozi***

___________________________
**Tarehe**

_______________________________
**Mkufunzi**